HALMASHAURI YA JIJI MWANZA

SHULE YA SEKONDARI MWANZA

MKUU WA SHULE - 0784 444 015 S.L.P. 149,
MATRON – 0784646528/0622233133 **MWANZA**
MAKAMU - 0682411929/0715013336/0752804469
mwanzasectz@gmail.com

Kumb Na; MZSS/S.034/FV/J.2022 29/03/2022

Jina la Mwanafunzi ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANZA HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA MKOA WA MWANZA MWAKA 2022/2023 – WASICHANA NA WAVULANA

(FOMU HII INA MAELEKEZO KWA WANAFUNZI WASICHANA NA WAVULANA)

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya ……..

2. **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Mwanza ipo umbali wa Kilometa 0.5 kutoka katikati ya mji wa Mwanza pembezoni mwa barabara ya kuelekea hospitali ya Rufaa ya Bugando. Usafiri wa tax au Pikipiki kutoka mjini unapatikana kwa nauli ya shilingi elfu moja (1000/=) kwa pikipiki na Shilingi elfu tatu (3000/=) kwa tax.

Aidha kwa wanafunzi wanaotoka nje ya mkoa wa Mwanza washukie kituo cha mabasi cha NATA kilicho takribani mita mia mbili (200) kutoka Shuleni.

3. **MUHULA WA MASOMO**

Muhula wa masomo unaanza tarehe **……** ,wanafunzi wa **BWENI** (wasichana) anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…….** na wa **KUTWA** (wavulana) tarehe ……... **HAKUNA MWANAFUNZI WA CHAGUO LA KWANZA ATAKAYE POKELEWA BAADA YA WIKI MBILI KUPITA TANGU SHULE IFUNGULIWE. SHULE ITAPOKEA WANAFUNZI WA CHAGUO LA PILI.**

4.0 MAELEKEZO KWA WASICHANA

. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WANAFUNZI WA BWENI**

4.1: SAREYA SHULE

a) Shati mbili za tetroni nzito nyeupe za mikono mirefu ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja upande wa kushoto . Zitavaliwa kwa kuchomekea.

- Sketi mbili ndefu zinazobakiza urefu wa inchi tano (05) kutoka kwenye kisigino cha mguu mpaka kwenye pindo la chini la sketi.
- Rangi ya sketi ni **Dark Green** Kitambaa cha Suti. Mshono ni Rinda Boksi moja kubwa mbele na nyuma na rinda za kawaida mbili kushoto na mbili kulia (mchoro wa mshono umeambatishwa)- kwenye utata fanya mawasiliano na shule kabla ya kushona.

- Iwe pana na isiyobana mwili.

C) Blauzi (Nusu Kanzu) kwa Waislam tu.
- Iwe ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono kitambaa cheupe cha tetron nzito.
- Iwe pana (isibane)
- Iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni)

➢ Kitambaa cha kichwani (ushungi)
- Kiwe kipana na cheupe
- Kiwe kirefu hadi kwenye vifundo vya viganja vya mikono,kisichofunika viganja vya mikono.
- Kisifunike uso
- Kisiwe chepesi

D) Nguo za kushindia (Shamba dress) ni gauni jozi mbili rangi ya **DARK BLUE (BLUU GIZA)** kitambaa cha suti zenye mshono wa rinda boksi mikono mirefu isiyobana kama ilivyo kwenye mchoro (mchoro wa mshono umeambatishwa) Urefu wa kwenda chini iwe sawa na urefu wa sketi ; **ushungi uwe ni maruni kitambaa kisicho cha suti.**

*E) Sare za michezo ni **raba nyeupe** na Track suit ya* **KIJIVU (GREY) NZITO** *(ADIDAS ISIYO YA MTEREZO) isiwe ya kubana mwili na pia iwe ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu.*

F) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vinavyo funika miguu vyenye visigino vifupi**.(visiwe "simple",buti au shingo ndefu)**

G) Soksi jozi mbili nyeupe ndefu zinazofika chini ya goti na zisizo na pambo lolote.

H) Tai moja ifanane na rangi ya sketi (dark green) na iwe na michirizi myeupe.

I) Sweta moja rangi ya **kijani** lenye michirizi myeupe shingoni, mikononi na chini isiyo **dariziwa**

J) Viatu vya kushindia ni vya wazi vya mpira(KOBAZ) rangi nyeusi zisizo na urembo.

K) T-SHIRT ya shule; fulana yenye nembo pamoja na motto ya shule.



Gauni la kushindia





5.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE KWA WASICHANA

S/NO	MAHITAJI	MHULA I	MHULA WA II	JUMLA
1	ADA	35,000/=	35,000/=	70,000/=
2	UKARABATI WA SAMANI	15,000/=		15,000/=
3	HUDUMA YA KWANZA (Kila mwanafunzi awe na bima ya	10,000/=	-	10,000/=
4	KITAMBULISHO NA PICHA	6,000/=	-	6,000/=
5	MAJI NA UMEME	10,000/=	-	10,000/=
6	NEMBO (sare za darasani)	2,000/=	-	2,000/=
7	WAFANYAKAZI WA MUDA	30,000/=	-	30,000/=
8	MITIHANI ENDELEZI	20.000/=		20,000/=
9	TAHADHARI(HAIREJESHWI)	5,000/=	-	5,000/=
10	TAALUMA	20,000/=	-	20,000/=
	JUMLA	153,000/=	35,000/=	188,000/=

NB: *BIMA YA AFYA YA NHIF KWA MWANAFUNZI ITAMUWEZESHA KUPATA MATIBABU YOTE IKIWA NI PAMOJA NA GHARAMA ZA KULAZWA PIA DAWA INAPATIKANA KWA TSHS 50,400/= KWA WANAFUNZI KWA MWAKA. KWA BIMA HII MWANAFUNZI ANAWEZA KUTIBIWA HOSPITALI YOYOTE ILIYOSAJILIWA NA MFUKO WA BIMA HAPA NCHINI. ILI KUPATA BIMA HIYO MZAZI AJAZE FOMU ZA MAOMBI TOKA OFISI YA BIMA NA ZITHIBITISHWE SHULENI KISHA AENDE ALIPIE KWENYE AKAUNTI YA MFUKO WA BIMA* ***(MZAZI ANAWEZAKUMPATIA MWANAE FEDHA KWA AJILI YA NHIF ALIPE AKIWA SHULENI)***

UTARATIBU WA MALIPO ADA NA MICHANGO

Shule haipokei fedha tasilimu. Malipo yote yafanyike kwenye akaunti za shule kupitia tawi lolote la NMB TANZANIA ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip)*** kama ifuatavyo:

a) Ada ilipwe kwenye akaunti: MWANZA SECONDARY SCHOOL ; A/C No 32201200007 NMB BENKI ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip).***
b) Michango mingine yote ilipwe kwenye akaunti: MWANZA SECONDARY SCHOOL a/c No 32910010534 NMB BANKI ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip).***

6.0 RATIBA YA KUTEMBELEA WANAFUNZI WA BWENI

Kutakuwa na ratiba ya kutembelea wanafunzi wa bweni mara **moja (01)** tu kwa muhula kuanzia **saa 4.00 (NNE) asubuhi** mpaka **saa 10.00 (kumi kamili)** jioni , tarehe 22/10/2022. Wataruhusiwa wazazi/walezi wenye picha zilizowekwa kwenye fomu hii ya kujiunga na shule kama ilivyelekezwa.

7.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO WASICHANA WANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

a) Ream za karatasi mbili (02) zilizoandikwa **Double A**

b) Godoro moja (01) upana futi 3 , urefu futi 6 : (zingatia vipimo vya godoro futi 3x6)
c) Shuka jozi mbili (02) zenye rangi ya PINK ziwe za COTTON (Pamba), foronya moja (01) rangi ya PINK, chandarua kimoja (01) cheupe cha pembe nne.

d) Scientific Calculator (FX-991 MS) Kwa wanafunzi wa tahasusi za PCB, PCM, PGM, CBG. CBN, EGM na HGE

e) Vifaa vya usafi binafsi kama taulo za kike, mswaki na dawa, sabuni, mafuta na "toilet paper" . **(Manukato, Cream za aina zote na vipodozi - haviruhusiwi)**

f) " Dissecting kit" kwa wanafunzi wa tahasusi za PCB, CBG na CBN.
g) "Dust coat" moja (01) nyeupe kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB, PCM, PGM,CBG na CBN **(Huvaliwa wakati wa "practica"l tu).**
h) Vyombo vya chakula (sahani na bakuli za **MFUPA**, kijiko , kikombe na chupa ya kutunzia maji ya kunywa-shule imefunga mfumo wa maji safi na salama ya kunywa unaotumiwa na jumuiya yote ya Mwanza Sekondari);
i) Vifaa vya usafi ; Kila mwanafunzi aje na mfagio mmoja **(01)** wa chelewa wenye mpini wa mti, mopa moja (01) ,ndoo moja ya lita kumi yenye mfuniko, kikombe cha kuogea pamoja na :
    - Soft Broom 01-(PCB,CBG,HGK na PGM),
    - Hard Broom 01- (HGE, na EGM)
    - Rubber Squizor 01 –(HGL,CBN,na PCM)
    - Brashi ngumu yenye mpini mfupi wa mbao/mti moja (01) kwa ajili ya kusafishia sinki la choo. Asilete yenye mpini wa plastic - (HKL)
j) Vitabu vya masomo ya **TAHASUSI (COMBINATION)** Husika
k) Kadi ya matibabu ya BIMA YA AFYA (NHIF) -inayoweza tumika hospitali yoyote ile.
l) Mpatie mwanao fedha chache kwa ajili ya mahitaji yake ya ziada.

m) Mnunulie sanduku la bati (trunker). Asije na begi/mabegi ya nguo za nyumbani, aje na trunker ndogo moja (01) tu.(**A**je na sanduku la bati lenye ukubwa wa wastani. Masanduku makubwa sana hayatapokelewa kwa sababu hakuna nafasi ya kuyatunza, atakaye kuja nalo atalazimika kulirudisha nyumbani kabla hajapokelewa shuleni.**)**

n) Aje na khanga au kitenge doti moja tu.

o) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na **kikoi** cha aina yoyote ile,shuka ya **kimaasai**, simu au laini ya simu, mtandio, kofia ya aina yoyote ile, viatu vya kushindia tofauti na vilivyoagizwa vya mpira. Atakayekujanavyo atachuliwa hatua za kinidhamu.

MUHIMU

Unaweza kupata mahitaji hayo kwenye maduka yaliyo karibu na shule ili kuepuka usumbufu wa mizigo mingi, tupo karibu kabisa na Soko kuu la jiji la Mwanza . VIFAA VYOTE VINAPATIKANA KATIKA MADUKA HAYO. UNAWEZA PIA KUSHONA NGUO KWENYE MADUKA HAYO.

MAELEKEZO KWA WAVULANA KIDATO CHA TANO –2022/2023

8.0 : SARE YA SHULE

a) Shati mbili nyeupe mikono mirefu, zinazofunika mifuko ya suruali, zisizobana.

b) Suruali mbili zenye marinda mawili nyeusi ndefu zinazofika chini ya vifundo vya miguu zenye mifuko mitatu. Upana wake chini miguuni usipungue **inch** 17-18.

(ZINGATIA – Ili kuepuka usumbufu wa kushona suruali nyingine)

L) Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vinavyo funika miguu vyenye visigino vifupi**.(visiwe buti au vyenye shingo ndefu)**

c) Sweta **Dark Blue** yenye michirizi myeupe shingoni, mikononi na chini kiunoni isiyodariziwa.

d) Tai moja nyeusi yenye michirizi myeupe.

e) Mkanda wa ngozi mweusi usio na urembo wa aina yoyote na chuma kikubwa.

f) T-SHIRT ya shule; fulana yenye nembo pamoja na motto ya shule.

9.0 ADA NA MICHANGO YA SHULE KWA WAVULANA

S/NO	MAHITAJI	MHULA I	MHULA WA II	JUMLA	AKAUNTI
1	ADA	10,000/=	10,000/=	20,000/=	**ADA**
2	UKARABATI WA SAMANI	15,000/=	-	15,000/=	**MICHANGO**
3	HUDUMA YA KWANZA (Kila mwanafunzi awe na bima ya afya)	5,000/=	-	5,000/=	
4	KITAMBULISHO NA PICHA	6,000/=	-	6,000/=	
5	NEMBO (sare za darasani)	2,000/=	-	2,000/=	
6	WAFANYAKAZI WA MUDA	20,000/=	-	20,000/=	
7	MITIHANI ENDELEZI	20.000/=	-	20,000/=	
8	TAHADHARI(HAIREJESHWI)	5,000/=	-	5,000/=	
9	TAALUMA	20,000/=	-	20,000/=	
	JUMLA	**103,000/=**	**10,000/=**	**113,000/=**	

NB: *BIMA YA AFYA YA NHIF KWA MWANAFUNZI ITAMUWEZESHA KUPATA MATIBABU YOTE IKIWA NI PAMOJA NA GHARAMA ZA KULAZWA PIA DAWA INAPATIKANA KWA TSHS 50,400/= KWA WANAFUNZI KWA MWAKA. KWA BIMA HII MWANAFUNZI ANAWEZA KUTIBIWA HOSPITALI YOYOTE ILIYOSAJILIWA NA MFUKO WA BIMA HAPA NCHINI. ILI KUPATA BIMA HIYO MZAZI AJAZE FOMU ZA MAOMBI TOKA OFISI YA BIMA NA ZITHIBITISHWE SHULENI KISHA AENDE ALIPIE KWENYE AKAUNTI YA MFUKO WA BIMA (**MZAZI ANAWEZA KUJA SHULENI KWA MAELEKEZO ZAIDI)***

UTARATIBU WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO

Shule haipokei fedha tasilimu. Malipo yote yafanyike kwenye akaunti za shule kupitia tawi lolote la NMB TANZANIA ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip)*** kama ifuatavyo:

a) Ada ilipwe kwenye akaunti: MWANZA SECONDARY SCHOOL ; A/C No **32201200007** NMB BENKI ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip).***

b) Michango mingine yote ilipwe kwenye akaunti: MWANZA SECONDARY SCHOOL a/c No **32910010534** NMB BANKI ***(andika jina kamili la mwanafunzi na kidato kwenye bank pay in slip).***

10: MAHITAJI MUHIMU AMBAYO WAVULANA WANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

a) Ream za karatasi mbili (02) Double "A"
b) "Box file" kubwa moja .
c) Scientific Calculator (FX-991 MS) Kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB, PCM, PGM, CBG. CBN,EGM na HGE
d) Dissecting kit kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB, CBG, PGM na CBN
e) Dust coat moja (01) nyeupe kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB, PCM, CBG,PGM na CBN **(Huvaliwa wakati wa practical tu).**
f) Vifaa vya usafi ; Kila mwanafunzi aje na mfagio mmoja**(01)** wa chelewa wenye mpini wa mti, ndoo moja ndogo ya lita kumi yenye mfuniko pamoja na :
   - Soft Broom 01-(PCB,CBG,HGK NA PGM),
   - Hard Broom 01- (HKL,HGE na EGM)
   - Rubber Squizor 01 –(HGL,PGM,CBN na PCM)

WANAFUNZI WOTE (WAVULANA NA WASICHANA)

11. Ni muhimu maelekezo yafuatayo yazingatiwe:

- **Mwanafunzi** atakayepata daraja sifuri au la nne ("DIVISION 0" AU "DIVISION IV") katika mitihani ya mwezi wa tisa-2022, kumi na mbili -2022, na mwezi wa nne-2023, hatoruhusiwa kwenda likizo husika, badala yake atabaki shuleni kuendelea na masomo.
- Mwanafunzi aje na "Result slip- NER" yenye matokeo yake ya kidato cha nne 2021
- Mwanafunzi aje na nakala ya cheti halisi cha kuzaliwa chenye majina kama yalivyo kwenye "Result Slip" na "sel-form"

12. MENGINEYO

Mwanafunzi anatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa kama ifuatavyo;

a) Anatakiwa kuwahi mara asikiapo kengele ya chakula.
b) Shule haina utaratibu wa utoaji wa chakula maalumu (special Diet), shule inajitahidi kutoa chakula kizuri na cha kuridhisha kwa wanafunzi wote kulingana na uwezo wa kifedha.
c) Mwanafunzi haruhusiwi kuleta au kuletewa chakula shuleni toka nje ya shule.
d) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na vitu kama vile simu ya mkononi, redio, pasi ya umeme na heater. Endapo atakamatwa na vitu kama hivyo atarudishwa nyumbani au hata kufukuzwa shule.
e) **IMANI**; **Madhehebu ambayo hayakurasimishwa na serikali** hayatatambuliwa shuleni isipokuwa kwa kibali maalumu cha serikali. Kila mwanafunzi ataruhusiwa kusali kwa utaratibu wa dhehebu lake kwa kuzingatia sheria za dhehebu lake na shule.
f) Mwanafunzi atavaa nguo rasmi muda wote ndani na nje ya shule, akiwa amevaa sare za shule mwanafunzi haruhusiwi kujiremba kwa kuvaa hereni, bangili, mikufu, kufuga kucha , kupaka kucha rangi, kupaka wanja, kuweka curl au relaxer ya nywele.

13: VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

Kabla ya mwanafunzi kufika shule ni lazima viambatisho vifuatavyo viwe vimejazwa kikamilifu.

a) Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaowe za kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

e) **Aje na "Result slip- NER" ya matokeo yake ya kidato cha nne 2021**.
f) **Nakala ya cheti halisi cha kuzaliwa chenye majina kama yalivyo kwenye vyeti vyako na "sel-form"**

13: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekele za Kikamilifu kabla ya kuja kuanza masomo.

- MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU BINAFSI SHULENI
- MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI LAINI AU VIFAA VYOVYOTE VYA SIMU SHULENI

ATAKAYE BAINIKA ATASIMAMISHWA MASOMO KISHA ATAFUKUZWA SHULE KWA MUJIBU WA TARATIBU ZA SHULE; HIVYO ASIJE NA SIMU WALA LAINI YA SIMU SHULENI-natambua wapo baadhi ya wanafunzi wasiokubali makatazo kama haya nawakumbusha tena wazingatie bila kudharau. (MAWASILIANO NA WAZAZI ATAFANYA KWA KUTUMIA SIMU YA MAKAMU MKUU WA SHULE, MATRON NA MWL WA MALEZI BILA MALIPO)

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWANZA

S.R. GEWA
MKUU WA SHULE

ADMN NO …… TAREHE YA KUINGIA …… SIMU …….. *Fomu mzss no. J2022/01*

PICHA YA MWANAAFUNZI

HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la Mwanafunzi(majina matatu aliyofanyia mtihani) ……
2. Shule ya Sekondari aliyosomea ……
3. Tarehe ya kuzaliwa ……
4. Dini/Dhehebu lake ……
5. Jina la Baba……. …….. (amefariki/yu hai)
6. Jina la mama……... …….. (amefariki/yu hai)
7. Anwani ya mzazi/wazazi ……
8. Jina la Mtaa/Kijiji ……
9. Jina la kitongoji……..… ……
10. Jina la Kata ……
11. Kazi aifanyayo baba ……
12. Simu ya baba……...
13. Kazi aifanyayo mama ……
14. simu ya mama…….
15. Namba ya simu ya nyumbani……

Simu yenye "whatsap" – weka vema (mama/baba/nyumbani)

Kama haishi na wazazi/mzazi.

16. Jina la Mlezi ……
17. Uhusiano na mlezi……..
18. Anwani ya mlezi ……
19. Simu Na……
20. Jina la mtaa/Kijiji…… ……..
21. Jina la kitongoji…… …….
22. Jina la Kata ……
23. Kazi aifanyayo mlezi ……
24. Namba ya simu ya nyumbani ……
25. Namba ya simu ya kazini/jirani ……
26. Namba nyingine ya familia yako……

27	**JINA LA NDUGU**	**JINSIA**	**UMRI**	**KAZI AIFANYAYO**	**ANAPOISHI**	**SIMU**	**SAINI**
1							
2							
3							
4							

28. Wewe ni mtoto wa ngapi katika familia yenu? .....
29. Jina la mlezi wako atakayepelekewa taarifa ya maendeleo yako ya taaluma na tabia kama si Baba au Mama ni ……...
    Uhusiano wako na Mlezi …….. …….
    Anwani yake …….
    Simu Na. itakayotumika kuwasiliana na mzazi …… ina "whatsap" (ndiyo/hapana)

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wazara ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia , yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshashaji Elimu.
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuandikishwa shuleni:-

1. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri kwa kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali ya umma.
10. Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba kitu chochote kile kikiwa ni cha mwenzake, mali ya shule au mali ya umma.
11. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya shule bila ruhusa.
12. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoheshimu picha za viongozi wa serikali, Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa (Coat of Arms). Wimbo wa Taifa, Fedha za Taifa na maandishi ya serikali.
13. Ni kosa kwa mwanafunzi kutosalimia au kutoonesha ukarimu kwa wakubwa wake katika kupokea mizigo na kujituma kusaidia katika shughuli mbalimbali.
14. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, walimu, wafanyakazi na kwa watu wengine ndani na nje ya shule.
15. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoitikia wito au kuchelewa mahali popote anapohitajika wakati wowote.
16. Ni kosa kwa mwanafunzi kutohudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
17. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia madawa ya kulevya (**mfano bangi na mirungi)** , kunywa pombe, kuvuta sigara au aina yoyote ile ya tumbaku pia, kuja na vitu vyenye ncha kali kama vile mkasi, kisu ,bisibisi na wembe.
18. Ni kosa kwa mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu na wafanyakazi, vilabu vya pombe, majumba ya kulala wageni na majumba ya starehe kama vile kumbi za dansi na video bila kibali maalum.
19. Ni kosa kwa mwanafunzi kufanya au kujihusisha na vitendo vya uasherati, kuoa au kuolewa.
20. Ni kosa kwa mwanafunzi kugombana, kupigana au kupiganisha.
21. Ni kosa kwa mwanafunzi kutovaa sare ya shule wakati awapo shuleni, kuonekana mchafu kwa kufuga ndefu, kucha, kunyoa kipara, kupaka rangi, kuvaa hereni, bangili, kofia, viatu vya gorofa, koti, rangi kuchani na mapambo ya aina yoyote.

22. Ni kosa kwa mwanafunzi kutosema ukweli au kutotoa ushahidi wa kweli wakati anapohitajika kufanya hivyo.
23. Ni kosa kwa mwanafunzi kuharibu usafi wa mazingira kama vile kujisaidia ovyo, kukatisha viwanja, kukata miti na kutupa takataka ovyo.
24. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni jumla ya siku 194 kwa mwaka .

NB: Makosa mbayo mwanafunzi akifanya anafukuzwa shule mara moja ni kama yafuatayo:-

1. **Wizi**
2. **Uasherati**
3. **Ulevi wa aina yoyote ile.**
4. **Utumiaji wa mdawa ya kulevya.**
5. **Makosa ya jinai.**
6. **Kupigana**
7. **Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.**
8. **Kudharau Bendera ya Taifa.**
9. **Kuoa na kuolewa.**
10. **Kupata mimba (wasichana) au kusababisha mimba (wavulana).**
11. **Kuharibu mimba (wasichana) ndani na nje ya shule.**
12. **Kugoma/kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.**
13. **Ubakaji.**
14. **Kukataa adhabu kwa makusudi.**
15. **Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.**

Mimi (jina kamili) ……. Nimesoma sheria za shule na kuzielewa na nitakapo zivunja nitakuwa nimetenda kosa hivyo niadhibiwe kwa mujibu wa kanuni na taratibu za shule.

Jina …….. Saini…… tarehe……..……

Fomu mzss no- J2022/03

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUKUBALIANA NA MAAGIZO NA SHERIA ZA SHULE.

Mimi ……. (Jina la Mwanafunzi). Nakubaliana na sheria na maagizo yote yaliyotolewa katika barua hii ya maelekezo. Naahidi kwamba kwa muda wote nitakaokuwa **MWANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI MWANZA** nitatii na kutekeleza sheria na taratibu zote za shule kwa dhati. (***Mwanafunzi atakaye gushi saini ya mzazi/mlezi ataadhibiwa naikiwezekana atafukuzwa shule kabisa , hivyo mzazi/mlezi aweke sahihi yake mwenyewe badala ya sahihi kuwekwa na mwanafunzi ili kuepusha usumbufu utakao jitokeza)***

JINA LA MWANAFUNZI ……..…….. SAINI ……..……

JINA LA MZAZI/MLEZI ……..…… SAINI …….simu ……

ina "whatsap" (ndiyo/hapana)

SAINI YA MKUU WA SHULE…….……. MHURI…….….

TAREHE ……..

Fomu mzss no- J2022/04

AHADI YA MZAZI KUSIMAMIA MWENENDO, MAHUDHURIO NA TAALUMA YA MWANAE SHULENI KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI YA MASOMO.

Mimi …… ambaye ni Mzazi/mlezi wa …….. ambaye ni (uhusiano) …… nakiri kukubaliana na sheria, kanuni, taratibu na maelekezo mengine yaliyotolewa na shule na kwamba natambua kuwa mwanangu anatakiwa kuhudhuria shule jumla ya siku 194 bila kukosa na pale atakapokuwa na tatizo ***nitaleta taarifa shuleni mara moja bila kuchelewa***. Endapo sitatoa taarifa nitakuwa nimetenda kosa la kumzuia kufika shuleni hivyo nitastahili kushitakiwa kwa kosa la uzembe wa kushindwa kumsimamia mwanangu kuhudhuria shuleni siku zote za masomo kwa mwaka, Pia nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma shuleni mara kwa mara.. (***Mwanafunzi atakaye gushi saini ya mzazi/mlezi ataadhibiwa na ikiwezekana atafukuzwa shule kabisa , hivyo mzazi/mlezi aweke saini yake mwenyewe badala ya saini kuwekwa na mwanafunzi ili kuepusha usumbufu utakao jitokeza)***

JINA LA MZAZI/MLEZI……..……SIMU Na……ina "whatsap" (ndiyo/hapana) **SAINI YA MZAZI ……..……. TAREHE ……**

Fomu mzss no. J2022/ 05

MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YAJINAI.

Mimi…… wa Mtaa/Kijiji……

Kitongoji cha …… Kata ya ……

Wilaya ya……Ambaye ni Mhitimu Elimu ya kidato cha nne toka Shule ya Sekondari ……Naahidi mbele ya Wazazi/ Walezi wangu ambao ni.

(a) Jina……Uhusiano……

(b) Jina……Uhusiano……

Kuwa kwa kipindi chote cha miaka miwili ninachotarajia kuwepo **shule ya Sekondari MWANZA** nikiwa kama Mwanafunzi kwa njia yoyote ile sitoanzisha wala kushiriki katika Migomo, fujo na kujihusisha katika makosa ya jinai, kwa kisingizio chochote kile; Kwani natambua kuwa matendo hayo husababisha hasara kubwa kwa Taifa, hivyo nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu shuleni na pale nitakapoona haki haitendeki nitatumia taratibu zilizowekwa ili haki itendeke na si vinginevyo.

Endapo nitakiuka ahadi hii natambua nitakuwa nimetenda kosa na nitastahili kufukuzwa shule kwani nitakuwa nimetenda kwa makusudi.

Jina la Mwanafunzi……saini……

1. Jina la mzazi……saini…… simu ……
2. Jina la mzazi……saini…… simu ……
3. Jina la mwenyekiti wa mtaa/kijiji ……simu ……Saini ……

   Tarehe …… Muhuri ……

SAINI YA MKUU WA SHULE…… Tarehe……

MHURI……

MAJINA NA PICHA ZA WAZAZI/WALEZI WATAKAO TAMBULIWA SHULENI

Picha ya mzazi au mlezi atakaye kutembelea shuleni

Jina :
Mahusiano:
Namba ya simu:
Saini :

Picha ya mzazi au mlezi atakaye kutembelea shuleni

Jina :
Mahusiano:
Namba ya simu:
Saini :

Picha ya mzazi au mlezi atakaye kutembelea shuleni

Jina :
Mahusiano:
Namba ya simu:
Saini :

Picha ya mzazi au mlezi atakaye kutembelea shuleni

Jina :
Mahusiano:
Namba ya simu:
Saini :

NAMBA YA MZAZI ITAKAYOTUMIKA KATIKA MAWASILIANO NA SHULE;(ni vema ikiwa na whatsap, pia ikibadilishwa taarifa zitolewe shuleni mara moja)

1……. **Ina "whatsap"** ndiyo/hapana

MWANZA SECONDARY SCHOOL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A: DATE ……

TO THE MEDICAL OFFICER

……
∗MR/ MISS …….
(Name in full)
Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for enrolment as a secondary school student. The examination should include the following categories:

I. (a) Eye – sight.
(b) Hearing.
(c) Limbs.
(d) Speech.
(e) Veneral diseases.
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
(h) Abdomen
(i) TB
II. Neuroses
III. Pregnancy.
IV. Other serious diseases

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Government Medical Officer).

I have examined the above named and consider that ∗he/ she is physically fit and mentally fit for enrolment as a secondary school student.

I (a) Eye – sight ……..……
(b) Hearing ……..……
(c) Limbs ……..……
(d) Speech ……..……
(e) Veneral diseases ……..……
(f) Leprosy ……..…
(g) Epilepsy ……..…
(h) Abdomen ……..…
(i) TB ……..…
II Neuroses ……..…
III Pregnancy ……..……
IV Other serious diseases ……..……
……
……
Medical Officers recommendations ……..……..
……..
……..
Date …… Signature ……..
Station …….. Designation ……..

∗***Delete as necessary.***

SIMU NA KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU HAVIRUHUSIWI SHULENI-UTAFUKUZWA SHULE @2022